# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WANAWAKE NA WATOTO -ZANZIBAR, APRILI MWAKA 2022

**Na: 04**

*Office of Chief Government Statistician*

*P.O. Box 2321, Zanzibar*
Telephone +255242231869
Email: zanstat@ocgs.go.com
Website: http://www.ocgs.go.tz

*Police Headquarter Zanzibar*

P.O.Box 237, PHQ Zanzibar
Fax No: 024223136
Email:cidhqznz@gmail.com

**Utangulizi**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kjinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


**Lengo**

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

**Matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia**

Jumla ya matukio 68 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Aprili, 2022. Kulikuwa na waathirika 69 ambao waathirika Wanawake ni tisa(9) (asilimia 13.0) na watoto ni 60 sawa na asilimia 87.0, miongoni mwao wasichana ni 48(asilimia 80.0) na wavulana ni 12 (asilimia 20.0).


**Kielelezo 1.1: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Aprili 2022**




**Chanzo: Makao** makuu ya Polisi –Zanzibar

Wilaya ya Magharibi "B" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 19), ikifuatia wilaya ya Mjini ambapo kumeripotiwa matukio 15. Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (tukio moja (1)) na wilaya ya Micheweni na Mkoani hakukuwa na tukio lolote lililoripotiwa katika wilaya hizo.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto kwa Wilaya, Aprili 2022**




**Chanzo:** Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi imepungua kwa asilimia 17.1 kutoka matukio 82 kwa mwezi wa Machi, 2022 hadi 68 mwezi wa Aprili, 2022. Aidha wilaya ya Magharibi "A" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Machi 2022 (matukio16) na wilaya ya Magharibi "B" imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Aprili 2022 (matukio19). Wilaya ya Kusini na Mkoani ziliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kwa mwezi wa Machi 2022 (matukio mawili (2) kwa kila wilaya) na wilaya ya Kaskazini "A" hakukuripotiwa tukio lolote. Ambapo wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (tukio moja (1)) na wilaya ya Micheweni na Mkoani hakukuwa na tukio lolote lililoripotiwa kwa mwezi Aprili 2022.

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Machi na Aprili 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 4 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 4 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 15 | 4 | 11 | 3 | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 7 | 15 | 3 | 3 | 1 | 2 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 |
| Magharibi 'A' | 16 | 9 | 5 | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 1 | 2 | 2 | 3 |
| Magharibi 'B' | 15 | 19 | 1 | 6 | 1 | 2 | 0 | 3 | 4 | 1 | 3 | 3 | 6 | 4 |
| Wete | 8 | 6 | 5 | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 6 | 5 | 2 | 1 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **82** | **68** | **41** | **28** | **8** | **9** | **4** | **12** | **13** | **1** | **6** | **8** | **10** | **10** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwaka imepungua kwa asilimia 37.0 kutoka matukio 108 kwa mwezi wa Aprili, 2021 hadi 68 mwezi wa Aprili, 2022. Wilaya ya Magharibi "A" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa mwezi Aprili, 2021 (matukio 57) ambapo wilaya ya Magharibi "B" imeongoza kwa mwezi wa Aprili, 2022 (matukio 19).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Aprili 2021 na Aprili 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 |
| Kaskazini 'A' | 5 | 4 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 4 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 9 | 4 | 6 | 3 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 15 | 0 | 3 | 2 | 2 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 57 | 9 | 8 | 4 | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 2 | 39 | 3 |
| Magharibi 'B' | 8 | 19 | 4 | 6 | 4 | 2 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 4 |
| Wete | 8 | 6 | 2 | 3 | 0 | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 6 | 3 | 2 | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **108** | **68** | **37** | **28** | **15** | **9** | **2** | **12** | **7** | **1** | **8** | **8** | **39** | **10** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Miongoni mwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia waliobakwa ni 28, wanawake walikuwa watatu (3) na wasichana ni 25; Waliolawitiwa walikuwa tisa (9), Kuingilia kinyume na maumbile ni 13 wote ni wasichana, Kutorosha alikuwa msichana mmoja(1), shambulio la aibu walikuwa nane (8) (wanawake ni wawili(2) na wasichana walikuwa sita (6)) na shambulio walikuwa 10 (wanawake ni wanne (4), wasichana watatu (3) na wavulana walikuwa watatu(3)).

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Aprili 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 15 | 3 | 2 | 7 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'A' | 6 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 16 | 5 | 2 | 3 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 6 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 7 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **60** | **25** | **9** | **13** | **1** | **0** | **6** | **0** | **3** | **3** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Aprili 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **9** | **3** | **0** | **0** | **2** | **4** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 24) sawa na asilimia 40.0 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka

6-10(matukio 22) sawa na asilimia 36.7. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 15) sawa na asilimia 60.0 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Aprili 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 0 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| 6-10 | | 4 | 6 | | | 9 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 22 |
| 11-14 | | 6 | 3 | | | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 12 |
| 15-17 | | 15 | 0 | | | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 3 | 24 |
| **Jumla** | | **25** | **9** | | | **13** | **0** | **1** | **0** | **6** | **3** | **3** | **60** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Aprili, 2022 imepungua kwa asilimia 13.0 (matukio 60) ukilinganisha na mwezi wa Machi, 2022 (matukio 69). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwezi uliopita imepungua kwa asilimia 33.3 kutoka matukio 36 kwa mwezi Machi 2022 hadi matukio 24 kwa mwezi wa Aprili 2022.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Machi na Aprili 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Machi 2022 | Jumla Aprili 2022 |
| | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | | |
| 0-5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| 6-10 | 0 | 4 | 5 | 6 | 2 | 9 | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 9 | 22 |
| 11-14 | 9 | 6 | 3 | 3 | 1 | 2 | 5 | 0 | 2 | 1 | 2 | 0 | 22 | 12 |
| 15-17 | 25 | 15 | 0 | 0 | 1 | 2 | 5 | 1 | 1 | 0 | 4 | 6 | 36 | 24 |
| **Jumla** | **34** | **25** | **8** | **9** | **4** | **13** | **12** | **1** | **5** | **6** | **6** | **6** | **69** | **60** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 33.3 kutoka matukio 36 kwa mwezi wa Aprili, 2021 hadi matukio 24 kwa mwezi wa Aprili, 2022, ambapo matukio katika umri wa miaka 6-10 yameongezeka kwa asilimia 10.0 kutoka matukio 20 kwa mwezi wa Aprili 2021 hadi matukio 22 kwa mwezi Aprili 2022.


**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Aprili 2021 na Aprili 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Aprili 2021 | Jumla Aprili 2022 |
| | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | | |
| 0-5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| 6-10 | 4 | 4 | 9 | 6 | 0 | 9 | 0 | 0 | 2 | 3 | 5 | 0 | 20 | 22 |
| 11-14 | 6 | 6 | 6 | 3 | 2 | 2 | 2 | 0 | 1 | 1 | 9 | 0 | 26 | 12 |
| 15-17 | 23 | 15 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 1 | 4 | 0 | 5 | 6 | 36 | 24 |
| **Jumla** | **34** | **25** | **15** | **9** | **2** | **13** | **6** | **1** | **7** | **6** | **19** | **6** | **83** | **60** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 42 kati ya matukio 68 yanaonekana yametokea sehemu nyengine sawa na asilimia 61.8 na matukio 26 yametokea nyumbani sawa na asilimia 38.2

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Sehemu Yaliyotokea, Aprili 2022**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa matukio yaliyotokezea sehemu nyengine kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 16.7 kutoka matukio 36 kwa mwezi wa Machi, 2022 hadi matukio 42 kwa mwezi wa Aprili, 2022, ambapo matukio yaliyotokea nyumbani yamepungua kwa asilimia 43.5 kutoka matukio 46 hadi matukio 26 kwa miezi hiyo.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Machi na Aprili 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Machi 2022 | Jumla Aprili 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | | |
| Nyumbani | 18 | 13 | 2 | 3 | 1 | 1 | 10 | 1 | 5 | 1 | 10 | 7 | 46 | 26 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 23 | 15 | 6 | 6 | 3 | 11 | 3 | 0 | 1 | 7 | 0 | 3 | 36 | 42 |
| **Jumla** | **41** | **28** | **8** | **9** | **4** | **12** | **13** | **1** | **6** | **8** | **10** | **10** | **82** | **68** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio yaliyotokea nyumbani kwa mwaka uliopita yamepungua kwa asilimia 44.7 kutoka matukio 47 kwa mwezi wa Aprili, 2021 hadi 26 mwezi wa Aprili, 2022 hata hivyo matukio yaliyotokea sehemu nyengine yamepungua kwa asilimia 31.1 kutoka matukio 61 hadi matukio 42 kwa miezi hiyo.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Aprili 2021 na Aprili 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Aprili 2021 | Jumla Aprili 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | | |
| Nyumbani | 17 | 13 | 1 | 3 | 2 | 1 | 4 | 1 | 4 | 1 | 19 | 7 | 47 | 26 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 20 | 15 | 14 | 6 | 0 | 11 | 3 | 0 | 4 | 7 | 20 | 3 | 61 | 42 |
| **Jumla** | **37** | **28** | **15** | **9** | **2** | **12** | **7** | **1** | **8** | **8** | **39** | **10** | **108** | **68** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 54 kati ya matukio 68 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi sawa na asilimia 79.4 na matukio 14 yapo Ofisi ya Mashtaka sawa na asilimia 20.6.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Hatua Zilizochukuliwa, Aprili 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 28 | 3 | 25 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 21 |
| Kulawiti | 9 | | | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 5 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 12 | 0 | 13 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 9 |
| Kutorosha | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 8 | 2 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| Shambulio | 10 | 4 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 |
| **Jumla** | **68** | **9** | **48** | **12** | **0** | **0** | **0** | **0** | **14** | **54** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Aprili 2022 ni 68 kati ya hao mmoja (1) alikuwa mume sawa na asilimia 1.5 na 67 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 98.5.

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Aprili 2022**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Aprili 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani | 13 | [redacted] | 13 | [redacted] | 3 | 3 | 1 | [redacted] | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 5 | 2 | 7 |
| Kazini | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 15 | [redacted] | 15 | [redacted] | 6 | 6 | 11 | [redacted] | 11 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 2 | 1 | 3 |
| **Jumla** | **28** | [redacted] | **28** | [redacted] | **9** | **9** | **12** | [redacted] | **12** | **1** | **0** | **1** | **8** | **0** | **8** | **7** | **3** | **10** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 15 | 3 | 2 | 7 | 0 | 1 | 2 |
| Magharibi 'A' | 9 | 4 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 |
| Magharibi 'B' | 19 | 6 | 2 | 3 | 1 | 3 | 4 |
| Wete | 6 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 6 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **68** | **28** | **9** | **12** | **1** | **8** | **10** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwezi Machi na Aprili 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 | Machi 2022 | Aprili 2022 |
| Kubaka | 41 | 28 | 7 | 3 | 34 | 25 | | |
| Kulawiti | 8 | 9 | | | | | 8 | 9 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 4 | 12 | 0 | 0 | 4 | 13 | | |
| Kutorosha | 13 | 1 | 1 | 0 | 11 | 1 | 1 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 6 | 8 | 1 | 2 | 4 | 6 | 1 | 0 |
| Shambulio | 10 | 10 | 4 | 4 | 1 | 3 | 5 | 3 |
| **Jumla** | **82** | **68** | **13** | **9** | **54** | **48** | **15** | **12** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwezi Aprili 2021 na Aprili 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Aprili 2021 | Aprili 2022 |
| Kubaka | 37 | 28 | 3 | 3 | 34 | 25 | | |
| Kulawiti | 15 | 9 | | | | | 15 | 9 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 2 | 12 | 0 | 0 | 2 | 13 | | |
| Kutorosha | 7 | 1 | 1 | 0 | 6 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 8 | 8 | 1 | 2 | 7 | 6 | 0 | 0 |
| Shambulio | 39 | 10 | 20 | 4 | 10 | 3 | 9 | 3 |
| **Jumla** | **108** | **68** | **25** | **9** | **59** | **48** | **24** | **12** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Zingatia Maelezo

**Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**

Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na:**

***Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***
***Sanduku la barua, 2321***
***Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz***

***Makao Makuu ya Polisi Zanzibar***
***Sanduku la barua, 237, MMP, Zanzibar***
***Barua pepe:cidphqznz@gmail.com***